**Ilani ya Faragha ya Tools for Humanity**

Asante kwa kuchagua kuwa mmoja wa Jamii ya World! World ni teknolojia huria, inayoungwa mkono na jamii ya kimataifa ya watengenezezaji programu, watu binafsi, na wachangiaji wengine.

Ilani hii ya Faragha inasimamia data unazotupatia kupitia matumizi yako ya tovuti, programu ("Programu"), mfumo wetu, na pia huduma nyingine zinazohusiana na Ilani hii ya Faragha (kwa pamoja, "Huduma"). Kauli hii ya Faragha imejumuishwa kwenye na inatawaliwa na Sheria na Masharti ya Mtumiaji ("Sheria za Mtumiaji"). Tools for Humanity Corporation ("TFH US"), pamoja na kampuni yake tanzu ya Ujerumani Tools for Humanity GmbH ("TFH Germany"; kwa pamoja, "**TFH**" au "**sisi**," "**yetu**"), inachangia kwenye utengenezaji na ukuzaji wa teknolojia ya World ("World") lakini ni tofauti na Asasi ya World ambayo inadhibiti uchakataji wa data zinazohusiana na kifaa cha Orb.

**1. Mdhibiti**

Sisi ni wadhibiti data wa "Data zote za Programu ya World", "Data za Kuthibitisha Stakabadhi" na "Data nyingine za Biashara": Tools for Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA. TFH ina kituo katika Umoja wa Ulaya (European Union, "**EU**") kupitia Tools for Humanity GmbH.

- "Data za Programu ya World" inamaanisha data zote za kibinafsi zilizokusanywa na kuchakatwa kupitia matumizi yako ya programu ya World App, kama ilivyobainishwa zaidi katika Sehemu ya 5 hapa chini, isipokuwa data zozote za kibinafsi zinazohusiana na matumizi yako ya mfumo wa World au sarafu za World (kama vile anwani yako ya pochi na data za miamala, ambazo hatukusanyi).
- Data za Kuthibitisha Stakabadhi inamaanisha data zinazochakatwa unapothibitisha maelezo ili kuyaongeza kwenye World ID yako ya umiliki wa kibinafsi. Hii inamaanisha K.m., kusoma kifaa cha NFC kwenye pasipoti yako ili kuhifadhi maelezo tako ya pasipoti kwenye kifaa chako. Data hizi ziko chini ya udhibiti wako na baada ya kuythibitisha uhalali wa stakabadhi yako, TFH inahifadhi kipande bila utambulisho cha kiwango cha hash cha sahihi ya kipekee ya kriptografia ya maelezo yako (k.m., pasipoti) ili kuhakikisha kwamba kila stakabadhi inaweza kuongezwa mara moja tu kwenye World ID.
- "Data za biashara" inamaanisha data zote za kibinafsi zilizokusanywa na kuchakatwa kupitia njia nyingine za kampuni yetu wakati wa kuwasiliana au njia yoyote nyingine ya kushirikiana au kutangamana nasi kupitia barua pepe, mikutano kwa video au tovuti zetu. Kwa uchakataji data katika muktadha wa Programu ya Orb tafadhali rejelea Ilani ya Faragha ya Programu ya Orb iliyounganishwa kwenye Programu ya Orb. Kwa uchakataji data katika muktadha wa ukusanyaji na majaribio ya data maalum tafadhali rejelea Ilani husika ya Faragha ya Ukusanyaji na Majaribio iliyounganishwa kwenye programu yako ya majaribio. Kwa uchakataji data katika muktadha wa tovuti yetu tafadhali rejelea Sera ya Kuki kwenye tovuti yetu.

**2. Visasisho vya Ilani hii ya Faragha**

Wakati mwingine tunasasisha Kauli hii ya Faragha. Tukifanya mabadiliko makubwa, kama vile jinsi tunavyotumia maelezo yako ya kibinafsi, basi tutakuarifu kupitia barua pepe au ujumbe katika Programu yako.

**3. Nini kiko ndani ya Kauli hii ya Faragha?**

- Jitihadi zetu za kulinda faragha yako na data zako
- Maelezo tunayokusanya na kwa nini
- Jinsi tunavyotumia data tunazokusanya
- Mahali ambako tunachakata data zako
- Wakati ambao tunashiriki data zako
- Jinsi data zako zinavyorekodiwa kwenye blockchain ya umma

- Jinsi tunavyotumia kuki
- Muda tunaohifadhi data zako
- Jinsi Ilani hii ya Faragha ilivyo tofauti kwa watoto na vijana
- Haki za kisheria ulizo nazo
- Jinsi ya kuwasiliana nasi kuhusu Ilani hii ya Faragha

**4. Jitihadi Zetu za Kulinda Faragha yako na Data zako**

Tunajitahidi kwa dhati kulinda faragha yako na kulinda data zako. Tunatambua kwamba tunaweza tu kutimiza misheni yetu ya kusambaza sarafu zetu za Kidijitali kwa njia ya haki kwa watu wengi kadri iwezekanavyo ikiwa watu watakuwa na imani nasi, na faragha na usalama wa data ni jambo la msingi ili kupata imani yako.

**Usiri**

Tumebuni bidhaa na huduma haswa tukijali faragha yako. Tunakusanya data ili kuboresha bidhaa na huduma zetu. Daima tutakueleza, hapa kwenye Kauli hii ya Faragha au katika fomu za idhini ya data za bidhaa na huduma maalum, ni data gani tunazokusanya, na kwa nini tunakusanya data hizo, na tunachofanya na data hizo.

**Usalama wa Data**

Tumeteua timu ya kutunza data zako na tumeweka kinga halisia na za kielektroniki zinazolinda data zako zinaposafirishwa na zinapohifadhiwa. Wakati huo huo, hakuna huduma inayoweza kuwa salama kabisa. Ikiwa una wasiwasi zozote kuhusu akaunti yako au data zako, tafadhali wasiliana nasi kupitia Lango letu la Maombi au kwa kututumia barua kwa anwani Tools For Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA.

**5. Maelezo Tunayokusanya na Kwa Nini**

**5.1 Data Unazotupatia**

Wewe kama mtumiaji, hauhitajiki kupatiana data zozote ili kufikia Programu. Hata hivyo, unaweza kuhitajika kutupatia data fulani ili uweze kutumia kipengele fulani ndani ya Huduma. Misingi ya kisheria ya kuchakata katika matukio yaliyo hapa chini ni idhini ya mtumiaji na utekelezaji wa mkataba (ahadi yetu ya kutoa Huduma). Hapa chini kuna orodha ya data unazoweza kupatiana na tunachoweza kufanya na data hizo:

Katika Muktadha wa Programu ya World:

- **Nambari ya simu.** Unaweza kuchagua kuweka nambari yako ya simu ili kuihusisha na akaunti yako. Kwa kibali chako, watumiaji wengine wanaweza kutafuta akaunti yako kwa kutumia nambari yako ya simu. Huenda tukahitaji nambari yako ya simu unapowasilisha ombi la data za mhusika. Misingi ya kisheria ya kuchakata data hizi ni utekelezaji Huduma chini ya Sheria za Mtumiaji.
- **Jina la Mtumiaji.** Unaweza kuunganisha jina la mtumiaji kwenye anwani ya pochi lako na kubadilisha jina la mtumiaji wakati wowote.
- **Tarehe ya Kuzaliwa.** Unaweza kufichua tarehe yako ya kuzaliwa ili kuhakikisha uambatanaji na vigezo vya umri unaohitajika. Hatutawahi kuhifadhi tarehe yako ya kuzaliwa lakini ni “checksum” ya data hizo na kama una umri wa zaidi ya miaka 18 au la.
- **Maoni na mawasiliano kutoka kwako.** Hii inajumuisha barua pepe zozote, ujumbe wowote, au mawasiliano mengine yoyote unayotutumia kupitia barua pepe au tovuti za mitandao ya kijamii ya wahusika wengine. Hii inaweza kujumuisha kuchakata anwani za barua pepe au wasifu za mitandao ya kijamii ikiwa unataka kuwasiliana nasi kupitia mbinu kama hizo. Tunaweza kutumia mtoa husuma mwingine ili kuwezesha utafiti kuhusu matumizi yako ya Huduma zetu. Misingi ya kisheria ya kuchakata data hizi ni utekelezaji Huduma chini ya Sheria za Mtumiaji.
- **Waasiliani kwenye kitabu cha waasiliani.** Unaweza kuruhusu Programu kufikia kitabu chako cha anwani ili kuwezesha kipengele

ambacho kinakurahisishia kutafuta na kutangamana na watumiaji wengine ambao huenda wakawa katika kitabu chako cha anwani. Misingi ya kisheria wa kuchakata data hizi ni nia halali ya mhusika kupatikana ndani ya Programu na nia ya mtumiaji aneyeshiriki kupata waasiliani wake ndani ya Programu.

**Tafadhali kumbuka:** Una jukumu la kuhakikisha kwamba kusambaza maelezo yako ya mawasiliano kunaambatana na sheria husika. Hii inaweza kukuhitaji upewe ruhusa na waasiliani wako na hautasambaza kwa TFH maelezo yoyote ya mawasiliano kutoka kwa watu wengine bila idhini yao ya moja kwa moja. Unaweza kubadilisha uamuzi wako na kuondoa uwezo wetu wa kufikia waasiliani wako wakati wowote katika mipangilio ya kifaa chako. Ukichagua kuleta waasiliani katika kitabu cha anwani cha kifaa chako kwenye Programu ili kujua ni waasiliani wagani wanatumia Huduma zetu au ili kuwaalika wajiunge nawe katika kutumia Huduma zetu, mara kwa mara tutalandanisha nambari za simu za waasiliani wako na nambari hizo na anwani husiani za pochi zilizopatianwa na watumiaji wengine kwenye seva setu.

- **Maelezo ya Eneo**. Unaweza kuamua kuwezesha huduma inayotegemea eneo (kama vile kipengele kinachokuruhusu kumpata Mhudumu wa Orb aliyekaribu nawe). Ni kwa idhini yako maalum pekee, tunaweza kukusanya maelezo kuhusu eneo lako kupitia GPS ili kuwezesha husuma inayotegemea eneo ili kukuonyesha kifaa cha Orb kilicho karibu nawe. Unaweza kubadilisha vibali vyako wakati wowote katika mipangilio ya kifaa chako. Ikiwa hayuko nchini Korea Kusini tunaweza pia kuhifadhi kadirio la eneo lako bila kuhusishwa na akaunti yako ya Programu ya World. Tunatumia data hizi ili kuboresha huduma zetu haswa lakini sio tu katika kuchagua maeneo ya kifaa cha Orb.
- **Soko la P2P**. Ikiwa unatumia Huduma za Soko la P2P (zinakopatikana) ambazo zinakuwezesha kununua sarafu za kidijitali kutoka kwa watumiaji wengine, basi tunaweza kuchukua maelezo ya ziada kama vile anwani yako ya pochi, maelezo yako ya mawasiliano, na nambari ya akaunti yako inayohusishwa na muamala (kama vile nambari yako ya M-PESA). Tunarekodi data za muamala kama sehemu ya kutoa Huduma za Soko la P2P. Pia tunaweza kuchukua maelezo ya ziada ili kuambatana na mahitaji husika ya KYC.
- **Metadata za kifaa.** Ikiwa unatumia Programu tunakusanya metadata kutika kwenye kifaa chako ili kuhakikisha kwamba Programu inafanya kazi vizuri na kwamba haukiuki Sheria na Masharti yetu. Hii inajumuisha kukusanya vitambulishi vya kifaa na anwani za IP.
- **Data za World ID za Kifaa.** Pia tunachakata metadata za kifaa chako ili kutathmini utambulisho wa kipekee wa kifaa. Msimbo wa utambulisho huu unatumika kama ishara inayothibitisha ubinafsi wako unapotumia World ID ya kifaa.

Katika muktadha wa uchakataji Data za Kibiashara:

- **Jina la kwanza na la mwisho.** Tunaweza kuchakata jina lako la kwanza na la mwisho ili kutimiza nia halali ya kudumisha na kudhibiti uhusiano wa kibiashara pamoja nawe.
- **Anwani ya Barua Pepe.** Pia unaweza kupatiana anwani yako ya barua pepe kwenye orodha yetu ya mapasho ili kufahamishwa kuhusu habari mpya za mradi wa World. Huenda tukahitaji anwani yako ya barua pepe unapowasilisha ombi la mmiliki data. Tunaweza kuchakata anwani yako ya barua pepe ili kutimiza nia halali ya kudumisha na kudhibiti uhusiano wa kibiashara pamoja nawe.
- **Nambari ya Simu.** Tunaweza kuchakata nambari yako ya simu ili kutimiza nia halali ya kudumisha na kudhibiti uhusiano wa kibiashara pamoja nawe.
- **Data za Biashara**. Ikiwa una uhusiano wa kibiashara nasi (kama vile wewe ni Mhudumu wa Orb au mletaji wetu), basi tunaweza kuhitaji maelezo kama vile majina, anwani ya barua, barua pepe, nambari ya simu, anwani ya pochi, na nyaraka zingine (kama vile kitambulisho chako cha serikali) kama sehemu ya kuimarisha uhusiano huo wa kibiashara na ili kutimiza majukumu ya kumjua-mteja-wako. Tunaweza kutumia huduma za wahusika wengine, kama vile Onfido, ili kutusaidia kukusanya na kuhakiki maelezo na nyaraka zilizotajwa hapa juu ili kutimiza majukumu ya kumjua-mteja-wako.
- **Data za utumaji ombi**. Ikiwa ungependa kufanya kazi nasi ni lazima ututumie ombi lako linalojumuisha barua ya kujieleza pamoja na CV na vile vile maelezo ya kibinafsi ambayo ungependa kufichua.

Unaweza kupata msingi wa kisheria wa kila shughuli ya kuchakata data hapa juu kwa kina zaidi kwenye **AMBATISHO LA I – Misingi ya**

**kisheria ya shughuli za Tools for Humanity za kuchakata data** mwishoni mwa ilani hii ya faragha.

**5.2 Data Tunazokusanya Kutoka Kwa Vyanzo Vingine**

Mara kwa mara, huenda tukapata maelezo kukuhusu wewe kutoka kwa vyanzo vingine vifuatavyo:

- **Data za Blockchain**. Tunaweza kuchambua data za blockchain ya umma ili kuhakikisha kwamba watu wanaotumia Huduma zetu hawajihusishi katika shughuli haramu au zilizopigwa marufuku chini ya Sheria za Mtumiaji, na ili kuchambua mitindo ya miamala kwa madhumuni ya utafiti na utengenezaji.
- **Huduma za Uthibitishaji Utambulisho**. Tunaweza kupata maelezo kutoka kwa huduma za wahusika wengine kwa kutumia data zako ili kuthibitisha utambulisho wako ikiwa inahitajika na sheria (kama vile mahitaji husika ya kumjua-mteja-wako). Ili kufafanua, **hatutumii** data zako za bayometriki tunapothibitisha utambulisho wako kama inavyohitajika na sheria.
- **Hifadhidata za talanta**. Huenda tukakusanya data kutoka kwa vyanzo mbali mbali ili kupeana kazi kwa watu walio na talanta.

**5.3 Data Tunazokusanya Kiotomatiki**

Tukiruhusiwa chini ya sheria husika, tunaweza kukusanya aina fulani za data kiotomatiki unapotumia Huduma zetu. Maelezo haya yanatusaidia kuangazia masuala ya uhudumiaji wateja, kuimarisha utendakazi wa Huduma, kukupa huduma fanisi na ya kibinafsi, na ili kulinda stakabadhi za Akaunti yako. Maelezo yanayokusanya kiotomatiki yanajumuisha:

- **Vitambulishi vya Mtandaoni:** Maelezo ya eneo la kijiografia (tazama hapa juu), mfumo msingi wa uendeshaji kompyuta au simu tamba, jina na toleo la kivinjari, na anwani za IP. Katika matukio chache sana data hizi pia zinawekwa katika rekodi yetu ya ugunduaji ulaghai na mtiririko haramu wa fedha. Pia vinahudumu kama njia ya kutoa huduma iliyostawi na bila ulaghai ya maunzitepe yetu.
- **Data za Matumizi:** Data za uthibitishaji, maswali ya kiusalama, na data nyingine zilizokusanywa kupitia kuki na teknolojia sawa.
- **Kuki**: faili ndogo za data zinazohifadhiwa kwenye hifadhi yako au kwenye kumbukumbu ya kifaa chako zinazotusaidia kuimarisha Huduma zetu na hisia zako, kuona ni maeneo na vipengele gani vya Huduma zetu ni maarufu, na kuhesabu mara unayotembelea Huduma. Ili kupata misingi ya kisheria ya kuchakata data hizo tafadhali rejelea Sera yetu ya Kuki ambapo tumeelezea aina tofauti ya kuki tunazotumia.

Hivyo hivyo, Programu inakusanya maelezo kwa ajili ya usuluhishaji matatizo na uimarishaji. Tunatumia huduma za wahusika wengine, kama vile Segment.io au PostHog, ili kufanya makadirio ya maelezo kuhusu matumizi ya watumiaji. Inapowezekana, tunachukua hatua ili kupunguza au kuficha maelezo yanayotumwa kwa wahusika wengine (kama vile kusimba data).

**5.4 Data Bila Utambulisho na Zilizokadiriwa**

Uondoaji utambulisho ni mbinu ya kuchakata data ambayo inageuza data kutozingatiwa kama data za kibinafsi kwani baada ya utambulisho kuondolewa data hizo haiwezi tena kuhusishwa na mtu fulani binafsi. Mifano ya data bila utambulisho zinajumuisha:

- Data za miamala
- Data za ubonyezaji maeneo ya skrini
- Metriki za utendakazi
- Vigunduaji ulaghai (ingawa data za kibinafsi zinatumika kwa malengo haya, pia)

Pia tunakadiria data, kwa kuunganisha pamoja viwango vikubwa vya maelezo ili yasimtambulishe tena wala kumrejelea mtu binafsi. Tunaweza kutumia data bila utambulisho au zilizokadiriwa kwa madhumuni yetu ya kibiashara, kama vile kuelewa mahitaji na tabia za watumiaji, kuimarisha Huduma zetu, kufanya shughuli za umaizi na uuzaji wa kibiashara. kugundua hatari za kiusalama, na kufunza teknolojia zetu.

Msingi wa kisheria wa kuchakata data zilizotajwa hapa juu ni nia halali ya kuwa na programu au tovuti inayofanya kazi, dhana za kibiashara na uzuiaji ulaghai.

**6. Jinsi Tunavyotumia Data Tunazokusanya**

**6.1 Maelezo Jumla**

Ni lazima tuwe na sababu halali (au "msingi wa kisheria wa kuchakata") ya kutumia maelezo yako za kibinafsi. Katika baadhi ya matukio, matumizi ya maelezo yako ya kibinafsi hayahitaji idhini yako ya mapema. Tunatumia data zako kwa malengo yafuatayo pekee:

- Kutoa na kudumisha bidhaa na huduma zetu chini ya Sheria za Mtumiaji. Huduma hizi zinajumuisha:
    - Programu ambapo watumiaji wanaweza kudhibiti World ID yao na sarafu zake za kidijitali na pia kujifunza kuhusu sarafu za kidijitali kwa ujumla na mradi wa World haswa;
    - Programu ya Mhudumu ambapo Wahudumu wa Orb wanaweza kudhibiti na kusimamia vifaa vyao vya Orb na takwimu za vifaa hivyo;
    - Soko la P2P ambapo tunapatanisha watumiaji na maajenti (haihusu watumiaji walio nchini Ujerumani au wana makazi yao au ofisi rasmi nchini Ujerumani);
- Kuimarisha na kutengeneza bidhaa na huduma zetu, ikijumuisha kuondoa hitilafu na kukarabati kasoro kwenye Huduma zetu.
- Kufanya utafiti wa sayansi ya data.
- Kuchambua matumizi yako ya Huduma zetu ili kukupa usaidizi bora.
- Kukuwezesha kuchapisha maelezo kwenye blockchain ili kuthibitisha wewe ni mtu binafsi.
- Kutumia anwani ya pochi lako ili kukutumia sarafu za kidijitali ambazo tunahusika nazo.
- Kuambatana na sheria husika kama vile sheria na vikwazo vya dhidi ya utakatishaji pesa. Hii inajumuisha:
    - Kutumia anwani yako ya IP ili kuwazuia watu binafsi kutoka mataifa au nchi zilizopigwa marufuku kutumia Huduma;
    - Kujibu maombi ya mmiliki data chini ya sheria husika za ulindaji data kama vile maombi ya kufikia au kufuta data;
    - Kufuatilia mitiririko ya fedha ambazo zinaweza kuwa chafu k.m. anwani zilizowekwa kwenye orodha nyeusi; na
- Kuambatana na sheria husika kama vile kanuni dhidi ya maudhui haramu.
- Kushughulikia maombi ya huduma, malalamishi na maswali yako kama mteja.
- Kusuluhisha migogoro, kutatua masuala, na kutekeleza makubaliano yetu nawe, pamoja na Ilani hii ya Faragha na Sheria za Mtumiaji.
- Kuwasiliana nawe kuhusiana na visasisho kwenye Huduma.

**6.2 Stakabadhi**

TFH inakuwezesha kuhifadhi maelezo fulani ya kuingia kwenye akaunti kwenye kifaa chako ili kuyasambaza katika muundombinu wa "zero knowledge" wa teknolojia ya World ID protocol ("Stakabadhi"). Katika muktadha wa Stakabadhi tunachakata data hizi kwa njia zifuatazo:

- Tunakagua uhalali wa stakabadhi yako (kama ni pasipoti hii inafanywa kupitia thibitisho la nchi yako).
- Tunakuthibitisha kama mmiliki halali wa stakabadhi hiyo (kwa pasipoti hii inafanywa kwenye kifaa chako kupitia picha ya uso wako (selfie) ambayo haihifadhiwi kamwe).
- Tunasimba, kuweka sahihi na kuhifadhi data za stakabadhi yako katika mazingira salama kwenye kifaa chako.
    - Hatuwezi kufikia maelezo ya kibinafsi yaliyo kwenye stakabadhi yako.
    - Kisha baadaye unaweza kusambaza maelezo haya na wahusika wanaohitaji kupitia ulinzi wa teknolojia ya World ID (k.m., unaweza kuthibitisha kwamba una umri wa anaglau miaka 18 bila kuvumbua umri wako haswa au wewe ni nani).

- Kwa pasipoti, TFH inadumisha tu maelezo bila utambulisho wa kiwango cha hash cha sahihi ya kipekee ya kriptografia ya pasipoti yako ili kuhakikisha kwamba kila pasipoti inaweza kuthibitishwa mara moja tu.

Uchakataji huu unategemea idhini yako na hatuwezi kufikia data zako za kibinafsi kutoka kwenye pasipoti yako ambazo zimehifadhiwa kwenye kifaa chako. Unaweza kufuta data hizi kwenye simu yako kwa kufuta Programu ya World.

**6.3 Data za World ID**

World ID yako (yaani nambari ya siri inayohitajika ili kuitumia) inahifadhiwa kwenye kifaa chako pekee (ikiwa una hifadhi rudufu kuna nakala iliyosimbwa ndani ya hifadhi rudufu yako). TFH au mwtu mwingine hawawezi kufikia World ID yako. Unaweza kutumia World ID yako bila kujitambulisha. Kila wakati unapotumia World ID kwenye programu mpya, programu hiyo inapokea tu nambari inayoweza kufutwa ("Kibatilishaji") ambayo haivumbui World ID yako. Hii inawezeshwa kupitia teknolojia ya "Zero Knowledge Proofs" (unathibitisha tu kuwa una World ID lakini si gani) na kuhakikisha kwamba World ID yako haiwezi kutumiwa kukufuatilia kwenye programu nyingi. Hii inamaanisha kwamba WorldID si kitambulisho jumla cha mtumiaji kwenye Intaneti.

World In inathibitisha utendaji kupitia teknolojia huria inayofikia "Merkle Tree" ya hadharani ya hash za World ID zilizothibitishwa. World ID si huduma yenye mamlaka kuu lakini ni teknolojia inayoweza kutumiwa na mtu yeyote. Tunatoa APIs ili kuwezesha ufikiaji wa "Merkle Tree" na World ID Proofs lakini hatupokei data zozote za kibinafsi katika muktadha huu.

Ni muhimu kukukbuka kwamba hatuchakati data zozote zinazohusiana na World ID yako ambazo zinaweza kutuwezesha kukutambulisha. Data zote za kibinafsi zinazochakatwa katika muktadha huu wa Programu ya World haswa anwani ya pochi lako na data za miamala zimepangwa kutohusishwa na data za World ID.

**7. Mahali Ambako Tunachakata Data Zako**

**7.1 Utumaji Data.**

Unapotupatia data zako, huenda zikatumwa, kuhifadhiwa, au kusindikwa katika eneo nje ya mahali ambako data zako zilikusanywa. Nchi ambako data zako zinatumwa, kuhifadhiwa, au kusindikwa huenda zikawa hazina sheria za ulindaji data ambazo ni sawa na zile za nchi ambako ulikuwa wakati ulipatiana data.

Tunafanya juhudi bora zaidi ili kuambatana na misimamo iliyotajwa katika kila eneo la mamlaka kuhusiana na sheria za faragha. Tunashiriki tu data na wasindikaji data walio nje ya eneo lako la mamlaka ikiwa utumaji huo wa data ni wa kisheria na ikiwa tuna imani kwamba msindikaji data huyo atalinda data zako kama inavyohitajika chini ya sheria husika na, aidha, kwa kuambatana na viwango vyetu.

**7.2 Hatari Zinazoweza Kukumba Utumaji Data**

Hapa chini ni orodha ya hatari zinazoweza kutokea tunapotuma data zako hadi Marekani, Umoja wa ulaya, au nchini nyingine. Hapa chini pia tumeweka muhtasari wa jinsi ya kuzuia hatari husika.

- Tunapofanya kadri tuwezayo ili kuhakikisha kwamba wanakandarasi wetu wadogo wana jukumu la kimkataba la kulinda data zako vya kutosha, wanakandarasi hawa wadogo huenda wasiwe chini ya sheria za faragha ya data za nchi yako. Wakandarasi wakichakata data zako kwa njia isiyo ya kisheria bila idhini, basi huenda ikawa vigumu kudai haki zako za faragha dhidi ya wakandarasi hao. Tunazuia hatari hii kwa kuwa na makubaliano dhabiti ya uchakataji data na wakandarasi wetu ambayo inawabidi kulinda data kwa kiwango cha GDPR na kutimiza maombi ya mhusika.
- Kuna uwezekano kwamba sheria ya faragha ya data nchini mwako haiendanishi na sheria za faragha ya data nchini Marekani, au katika EU. Daima tutajaribu kuambatana na kiwango cha juu zaidi cha ulindaji data ambacho tunatumia.
- Kuna uwezekano kwamba data zako zitaweza kufikia na maafisa au mamlaka za kiserikali. Katika matukio hayo tumejitayarisha kupinga mahakamani ombi lolote la kiserikali la kufikia data ambalo si halali, linapita mipaka, au si la kisheria. Aidha tunatumia usimbaji wa hali ya juu ili kuzuia ufikiaji bila idhini.

Tafadhali kumbuka kwamba orodha hii ina mifano, lakini huenda haijajumuisha hatari zote zinazoweza kukukumba.

**7.3 Mfumo wa Faragha ya Data kwa utumaji data Marekani**

TFH inaambatana na Mfumo wa Faragha ya Data wa EU-U.S. (EU-U.S. DPF), Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF, na Mfumo wa Faragha ya Data ya Swiss-U.S. (Swiss-U.S. DPF) kama ilivyobainishwa na Idara ya Biashara ya Marekani. TFH imethibitishia Idara ya Biashara ya Marekani kwamba inaambatana na Kanuni za Mfumo wa Faragha ya Data za EU-U.S. (EU-U.S. DPF Principles) kuhusiana na uchakataji wa data za kibinafsi zilizopokewa kutoka kwa Umoja wa Ulaya kwa kutegemea EU-U.S. DPF na zilizopokewa kutoka Uingereza (na Jibrata) kwa kutegemea Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF. TFH imethibitishia Idara ya Biashara ya Marekani kwamba inaambatana na Kanuni za Mfumo wa Faragha ya Data za Swiss-U.S. (Swiss-U.S. DPF Principles) kuhusiana na uchakataji wa data za kibinafsi zilizopokewa kutoka Uswizi kwa kutegemea Swiss-U.S. DPF. Ikiwa kuna ukinzani wowote kati ya masharti yaliyo katika Ilani hii ya Kanuni za Faragha ya Data na Kanuni za DPF ya EU-U.S. na/au Kanuni za DPF ya Swiss-U.S. DPF Principles, kanuni hizo zitatawala. Ili kujua mengi zaidi kuhusu mpango wa Mfumo wa Faragha ya Data (Data Privacy Framework, DPF), na ili kutazama thibitisho letu, tembelea https://www.privacyshield.gov/.

TFH ina wajibu wa kuchakata data za kibinafsi ambazo inapokea chini ya DPF na kisha kuzituma kwa wahusika wengine ambao ni maajenti wake. TFH inaambatana na Kanuni za DPF kwa utumaji wote wa data za kibinafsi kutoka EU, Uingereza, na Uswizi, pamoja na kauli a dhima ya utumaji.

Tume ya Baishara ya Kitaifa ina mamlaka juu ya uambatanaji wa TFH na EU-U.S. DPF, Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF, na pia Swiss-U.S. DPF. Katika hali fulani, TFH inaweza kuhitajika kufichua data za kibinafsi katika kujibu maombi ya kisheria kutoka kwa mamlaka za umma, pamoja na kutimiza vigezo vya usalama wa kitaifa au utekelezaji sheria.

Katika kuambatana na EU-U.S. DPF na Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF na pia Swiss-U.S. DPF, TFH inajitahidi kusuluhisha malalamishi yanayohusiana na Kanuni za DPF kuhusu ukusanyaji na matumizi yetu ya maelezo yako ya kibinafsi.. Watu wa EU na Uingezeza na Uswizi walio na maombi au malalamishi kuhusiana na jinsi tunavyoshughulikia data za kibinafsi zilizopokewa kwa kutegemea EU-U.S. DPF na Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF na pia Swiss-U.S. DPF kwanza wanapaswa kuwasiliana na TFH kwa anwani dpo@world.org

Katika kuambatana na EU-U.S. DPF na Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF na pia Swiss-U.S. DPF, TFH inajitahidi kushirikiana na kuambatana na ushauri wa jopo lililotengenezwa na mamlaka za ulinzi wa data za EU (Data Protection Authorities, DPAs)} na Ofisi ya Kamishna wa Maelezo (Information Commissioner's Office, ICO) wa Uingereza na Mamlaka ya Udhibiti ya Gibraltar (Gibraltar Regulatory Authority, GRA) na Kamishna wa Ulinzi wa Data na Maelezo wa Kitaifa (Federal Data Protection and Information Commissioner, FDPIC) wa Uswizi kuhusiana na ushughulikiaji wa data za kibinafsi zilizopokewa kwa kutegemea EI-U.S. DPF na Nyongeza ya Uingereza kwenye EU-U.S. DPF na pia Swiss-U.S. DPF.

Kwa malalamishi kuhusiana na uambatanaji na DPF ambayo hayajasuluhishwa na mbinu nyingine zozote za DPF, una wajibu, chini ya hali fulani, kuagiza mchakato wa usuluhishaji. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana kwenye tovuti rasmi ya DPF.

**8. Wakati ambao Tunashiriki Data Zako**

**Hatutawahi kuuza data zako**.

Wakati ambapo tunasambaza data zako nje ya shirika letu, kila wakati:

- Tunazishiriki kwa njia salama;
- Kuchukua hatua kuhakikisha kwamba inashughulikiwa kwa njia ambayo inaendanisha na jitihada zetu kwa faragha yako; na
- Tunazuia kampuni zingine kutozitumia kwa malengo yao binafsi.

Tunasambazai data zako kwa njia hizi chache:

- **Tunazambazia Asasi ya World:** Tunaweza kutenda kama wachakataji wa Asasi ya World wa data za kibinafsi kwa niaba ya World (tafadhali tazama kauli ya faragha ya World ili kupata maelezo zaidi).
- **Kusambaza ndani ya shirika letu:** Tunafichua tu data kwa wanatimu wetu ambao wanahitaji kuzifikia ili kuweza kufanya kazi na majukumu yao. Tunafichua tu kiwango cha data ambacho kinahitajika ili kufanya kazi na majukumu fulani na kuwa na mfumo ulio na udhibiti mkali wa ufikiaji.
- **Kusambaza kwa wachuuzi na watoa huduma nje ya shirika letu:** Tunafichua tu data kwa watoa huduma ambao huduma zao

tunazitegemea ili kuchakata data na kukupa Huduma zetu. Tunafichua tu data kwa wachuuzi wa huduma ya uthibitishaji utambulisho ikiwa inahitajika na Sheria (yaani, mahitaji-ya-kumjua-mteja-wako).

- Kategoria za watoa huduma hao ni:
- Watoa huduma ya wingu (aina zote za data)
- Watoa bidhaa za SaaS; tunatumia bidhaa za SaaS katika kategoria zifuatazo:
    - Menejimenti ya hifadhidata na miundombinu
    - Usalama wa Data
    - Uteuzi
    - Mawasiliano
    - Utafiti
    - KYC/KYB yaani. kukagua hati rasmi
    - Menejimenti ya maombi ya data
    - Usaidizi wa kiufundi
    - Huduma kwa watumiaji
- Wataalamu wa nje
    - Watengenezaji maunzitepe maalum
    - Wataalamu wa kisheria
    - Washauri wa ushuru
- Benki
- Watoa huduma ya kuweka lebo (chini ya ulinzi maalum pekee)
- Huduma za ukaguaji historia za watumaji maombi na Wahudumu wa Orb
- **Kwa watekelezaji sheria, maafisa, au wahusika wengine:** Tunaweza kufichua data zako ili kuambatana na sheria husika na kutii mahitaji ya lazima ya kisheria. Kwa uangalifu tunazingatia kila ombi ili kubaini kana kwamba ombi hilo linaambatana na sheria na, panapofaa, tunaweza kupinga maombi ambayo si halali, yanayopita mpaka, au yasiyo ya kisheria. Tunaweza kushiriki data za kibinafsi na polisi na mamlaka nyingine za serikali ambapo tunaamini ni muhimu ili kuambatana na sheria, kanuni au mchakato au jukumu nyingine la kisheria.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi ikiwa tunaamini kwamba matendo yako hayaendanishi na Sheria zetu za Mtumiaji, ikiwa tunaamini kwamba umekiuka sheria, au ikiwa tunaamini kwamba ni muhimu ili kulinda haki zetu, mali yetu, na usalama wetu, watumiaji wetu, umma, na wengine.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi na mawakili wetu na washauri wengine wataalamu ambapo ni muhimu ili kupata ushauri au vinginevyo kulinda na kudhibiti bia zetu za kibiashara.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi kuhusiana, au wakati wa majadiliano kuhusiana na, ununuzi wowote, mali ya kampuni kuuzwa, ufadhili, au sehemu ya biashara au biashara yote kununuliwa na kampuni nyingine.
- Data, ikijumuisha maelezo yako ya kibinafsi, zinaweza kushirikiwa miongoni mwa kampuni mzazi, washirika, na kampuni tanzu za siku zijazo na kampuni nyingine chini ya udhibiti na umiliki wa pamoja.
- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya kibinafsi kwa idhini yako au kwa maagizo yako.

**9. Jinsi Data Zako Zinavyorekodiwa kwenye Blockchain ya Umma**

Maelezo ya miamala yanayohusiana na matumizi yako ya Huduma zetu yanaweza kurekodiwa katika blockchain ya umma.

**Tafadhali kumbuka:** Blockchain ni rekodi ya hadgharani ya miamala ambazo zinadumuishwa kwenye mitandao isiyo na mamlaka kuu inayoendeshwa na wahusika wengine ambayo haidhibitiwi wala kuendeshwa na World. Kwa ajili ya hali ya rekodi za blockchain kuwa za umma na zisizoweza kubadilishwa, hatuwezi kutoa hakikisho la uwezo wa kurekebisha, kufuta, wala kudhibiti ufichuaji wa data zilizopkiwa na kuhifadhiwa kwenye blockchain

**10. Jinsi Tunavyotumia Kuki**

Tunatumia kuki ili kusaidia Huduma zetu kufanya kazi vyema zaidi. Kando na kuki, tunaweza kutumia teknolojia nyingine sawa na hiyo, kama vile web beacons, ili kuwafuatilia watumiaji wa Huduma zetu. Web beacons, (pia zinaitwa "clear gifs") ni grafiki ndogo sana zilizo na kitambulishi cha kipekee, zilizo na utendaji sawa na kuki. Sera yetu ya Kuki, imejumuishwa hapa kama rejeleo.

Pia tunatumia huduma ya Google Analytics. Maelezo mengi zaidi kuhusu jinsi Google inavyotumia data zako unapotumia tovuti na programu za wabia wake: https://policies.google.com/technologies/partner-sites. Kwa kutumia Huduma hizi, unatuidhinisha kuhifadhi na kufikia kuki na data nyingine kwenye kompyuta yako au kifaa chako tamba na kutumia huduma ya Google Analytics kuhusiana na shughuli hizo. Tafadhali soma maelezo yaliyo kwenye kiungo kilichopatianwa ili uelewe unachoidhinisha.

**11. Tunahifadhi Data Zako Kwa Muda Gani?**

Isipokuwa iwe imetajwa vinginevyo na sheria husika, tunahifadhi data zako kwa muda ambao unahitajika ili kukupa Huduma zetu, kutimiza malengo yetu ya kibiashara, na kuambatana na majukumu yetu ya kisheria na kiudhibiti. Ukifunga akaunti yako, tutafuta data za akaunti yako ndani ya mwezi mmoja; vinginevyo tutafuta data za akaunti yako baada ya miaka 2 ya kukosa shughuli. Ikiwa inahitajika na sheria, tutaendelea kuhifadhi data zako za kibinafsi kadri inavyohitajika ili kuambatana na majukumu yetu ya kisheria na kiudhibiti, pamoja na kufuatilia, kugundua, na kuzuia ulaghai, na pia majukumu ya ripoti za ushuru, uhasibu, na kifedha.

**Tafadhali kumbuka:** Blockchain ni mitandao ya wahusika wengine ambayo hatudhibiti wala kuendesha. Kwa ajili ya hali ya teknolojia ya blockchain kuwa ya umma na isiyoweza kubadilishwa, hatuwezi kurekebisha, kufuta, wala kudhibiti ufichuaji wa data zilizohifadhiwa kwenye blockchain.

**12. Jinsi Ilani hii ya Faragha ilivyo Tofauti kwa Watoto na Vijana**

Watu chini ya umri wa miaka 18 hawaruhusiwi kutumia Huduma, na hatukusanyi data kutoka kwa watu walio na umri wa chini ya miaka 18. Ikiwa unaamini kwamba mtoto wako aliye chini ya umri wa miaka 18 amefikia Huduma bila kibali chako, unaweza kuomba data zake kufutwa kwa kuwasiliana nasi kupitia Lango letu la Maombi.

Tukijua kwamba tumekusanya data kumhusu mtoto chini ya umri wa miaka 18, tutafuta data hizo haraka iwezekanavyo. Tumechukua hatua kama vile kuweka teknolojia ya AI ya kugundua umri kiotomatiki, maagizo kwa wahudumu na uthibitisho wa mtu binafsi ili kuwekea vikwazo matumizi ya Huduma kwa watu walio na umri wa angalau miaka 18. Hatutengenezi bidhaa au huduma za sokoni kwa ajili ya watoto.

**13. Jinsi ya Kuwasiliana Nasi kuhusu Ilani hii ya Faragha**

Pia unaweza kuchagua kufuta data zako kutoka kwenye ndani ya Programu chini ya menyu ya Mipangilio. Ikiwa una maswali au wasiwasi zozote kuhusu Ilani hii ya Faragha, ungependa kutumia haki zako, au kuwasiliana na Afisa wa Ulinzi wa Data, tafadhali wasilisha ombi lako kupitia Lango letu la Maombi au kwa kututumia barua kwa anwani Tools For Humanity Corporation, 548 Market Street, PMB 49951, San Francisco, CA 94104 USA au dpo@toolsforhumanity.com. Tutajibu maombi yote yunayopokea kutoka kwa watu wanaotaka kutumia haki zao za ulindaji data kulingana na sheria husika za ulindaji data. Pia unaweza kufuta data zako kutoka kwenye ndani ya Programu ya World.

Ikiwa una wasiwasi zozote za faragha au matumizi data ambazo hazijasuluhishwa na ambazo hazikushughulikiwa mpaka ukaridhika, tafadhali wasiliana na mdhibiti ulinzi wa data katika eneo lako. Ikiwa unaishi EU, basi unaweza kupata mdhibiti ulinzi wa data wako hapa.

**14. Haki Zako**

Haki hizi zinatumika pale tu ambapo tunaweza kumtambulisha mwombaji katika hifadhidata yetu na pale tu ambapo hatukiuki haki zingine za mmiliki data kwa kutekeleza haki za mwombaji:

- Una haki ya kupata kutoka kwetu wakati wowote baada ya kutuma ombi maelezo kuhusu data za kibinafsi tunazochakata kukuhusu. Una haki ya kupata kutoka kwetu data za kibinafsi zinazokuhusu.
- Una haki ya kuagiza kwamba mara moja tusahihishe data za kibinafsi zinazokuhusu ikiwa si sahihi.
- Una haki ya kuagiza kwamba tufute data za kibinafsi zinazokuhusu. Mahitaji haya yanaonyesha haki ya kufutwa ikiwa data za kibinafsi si muhimu tena kwa madhumuni ambayo ilifanya zikusanywe au kuchakatwa, mradi mahitaji ya kufuta chini ya sheria husika yamebainishwa (k.m. sheria kadhaa za maeneo ya mamlaka zinatuhitaji kuhifadhi maelezo ya miamala kwa kipindi fulani cha muda)
- Una haki ya kuondoa kwa hiari idhini yako ya uchakataji wowote wa data kwa idhini au kukataa uchakataji wa data ikiwa si kwa idhini.

**15. HATI ZA NYONGEZA**

Ifuatayo, hati kadhaa za nyongeza zinatoa maelezo yanahitajika kisheria kwa masoko husika ambapo tunaendesha shughuli. Maelezo haya ni sehemu ya idhini kulingana na eneo ambako mmiliki data anaishi. Maelezo haya yanaweza kutofautiana na maelezo ya eneo lako kwa sababu tunazuilia huduma fulani katika maeneo fulani ya mamlaka. Endapo kuna tofauti na yaliyo hapa juu kauli maalum kuhusu eneo fulani la mamlaka inatumika:

**Nyongeza ya A: Eneo la Kiuchumi la Ulaya (“EEA”) na Uingereza (“UK”)**

Ikiwa upo katika EEA au UK yafuatayo yanatumika kwako: Una angalau haki zifuatazo. Unaweza kuwa na haki za ziada chini ya Kanuni Jumla za Ulinzi wa Data, Kanuni ya EU ya 2016/679 ya 27.04.2016 (“GDPR”) kama ilivyoorodheshwa hapa chini. Ili kutumia haki zako zinazopatikana chini ya GDPR, tafadhali wasiliana nasi kwenye Lango letu la Maombi. Kando na matukio ya kipekee, tutajibu ombi lako ndani ya makataa ya kisheria ya mwezi mmoja. Matumizi ya neno GDPR katika sehemu ifuatayo pia yanajumuisha UK-GDPR iliyojumuishwa katika sheria za kitaifa za Uingereza kama Sheria ya UK ya Ulinzi wa Data ya 2018 na kuhifadhiwa kama sehemu ya sheria za Uingereza na Wales, Scotilandi na Ayalandi Kaskazini kwa Sehemu ya 3 ya sheria ya European Union (Withdrawal) Act 2018 na kama ilivyorekebishwa na Schedule 1 kwenye Data Protection, Privacy and Electronic Communications (Amendments etc) (EU Exit) Regulations 2019 (SI 2019/419).

**A.1 Haki za kisheria chini ya GDPR**

Sehemu hii inatumika ikiwa uchakataji data zako upo chini ya wigo wa matumizi ya GDPR (*k.m.*, ikiwa wewe ni mkaazi katika EEA au nchini UK). Huenda ikawa una haki za ziada chini ya GDPR kama ilivyoorodheshwa hapa chini. Ili kutumia haki zako zinazopatikana chini ya GDPR, tafadhali wasiliana nasi kwenye Lango letu la Maombi.

- Una haki ya kupata kutoka kwetu wakati wowote baada ya kutuma ombi maelezo kuhusu data za kibinafsi tunazochakata kuhusiana na ndani ya wigo wa Kifungu cha 15 cha GDPR.
- Una haki ya kuagiza kwamba mara moja tusahihishe data za kibinafsi zinazokuhusu ikiwa si sahihi.
- Una haki, chini ya hali zilizoelezewa katika Kifungu cha 17 cha GDPR, kuagiza kwamba tufute data za kibinafsi zinazokuhusu. Mahitaji haya yanaonyesha haki ya kufutwa ikiwa data za kibinafsi si muhimu tena kwa madhumuni ambao ilifanya zikusanywe au kuchakatwa, na pia katika matukio ya uchakataji usio wa kisheria, uwepo wa pingamizi au uwepo wa jukumu la kufuta chini ya sheria la Umoja au sheria ya Jimbo kwa ambayo tupo chini yake.
- Una haki ya kuagiza kwamba tuwekee vikwazo uchakataji kulingana na Kifungu cha 18 cha GDPR.
- Una haki ya kupokea kutoka kwetu data za kibinafsi zinazokuhusu ambazo umetupatia kwa umbizo sambamba, linalotumika kwa kawaida, na linalosomeka na mashine kulingana na Kifungu cha 20 cha GDPR.
- Wakati wowote, kwa misingi inayohusiana na hali yako haswa, una haki ya kupinga uchakataji wa data za kibinafsi zinazokuhusu ambao umefanywa, na kadhalika, kwa misingi ya Kifungu cha 6 (1) sentensi ya 1, eneo la f kwenye GDPR,

kulingana na Kifungu cha 21 cha GDPR.

- Una haki ya kuwasiliana na mamlaka adilifu ya usimamizi endapo kutakuwa na malalamishi kuhusu uchakataji data unaofanywa na mdhibiti. Mamlaka ya usimamizi inayowajibika ni: the Bavarian State Office for Data Protection Supervision (Bayerisches Landesamt für Datenschutz).
- Ikiwa uchakataji wa data za kibinafsi unategemea idhini yako, una haki chini ya Kifungu cha 7 cha GDPR una haki ya kughairi idhini yako ya matumizi ya data zako za kibinafsi wakati wowote katika siku zijazo, ambapo kughairi huku ni rahisi kufanya kama ilivyo kuwa rahisi kupatiana idhini. Tafadhali kumbuka kwamba kughairi kunaathiri tu siki zijazo. Uchakataji uliofanyika kabla ya kughairi hauathiriki.

**A.2 Utumaji Data**

- Tunapotuma data hadi kwenye nchi ambayo hatuna uamuzi wa utoshelevu, tunatumia EU Standard Contractual Clauses (Vipengee vya Kimkataba vya Kawaida vya EU). Kwa sasa tunatuma tu data za kibinafsi hadi Marekani.
- Ikiwa uchakataji wa data za kibinafsi unategemea idhini yako, una haki chini ya Kifungu cha 7 cha GDPR una haki ya kughairi idhini yako ya matumizi ya data zako za kibinafsi wakati wowote katika siku zijazo, ambapo kughairi huku ni rahisi kufanya kama ilivyo kuwa rahisi kupatiana idhini. Tafadhali kumbuka kwamba kughairi kunaathiri tu siki zijazo. Uchakataji uliofanyika kabla ya kughairi hauathiriki. Tafadhali pia kumbuka kwamba kuchakata hayo hakutegemei idhini na hivyo hakuathiriki na uondoaji idhini.

**NYONGEZA YA B: JAPANI**

Ikiwa unaishi Japani, aidha, yafuatayo yanatumika kwako.

**B1. Maelezo Kuhusiana na Kanuni za Japani**

Tunaambatana na sheria na kanuni za Japani, pamoja na Sheria ya Japani ya Ulinzi wa Maelezo ya Kibinafsi (Act on the Protection of Personal Information, "APPI"). Sehemu hii inatumika katika jinsi tunavyoshughulikia "maelezo ya kibinafsi" kama ilivyobainishwa katika APPI kwa pamoja na sehemu nyingine za Fomu hii ya Idhini ya Data za Bayometriki

Tunaambatana na sheria na kanuni za Japani, pamoja na Sheria ya Japani ya Ulinzi wa Maelezo ya Kibinafsi (Act on the Protection of Personal Information, "APPI"). Sehemu hii inatumika katika jinsi tunavyoshughulikia "maelezo ya kibinafsi" kama ilivyobainishwa katika APPI kwa pamoja na sehemu nyingine za Ilani hii ya Faragha.

**B2. Kusambaza Data**

Isipokuwa iwe imeruhusiwa vinginevyo na sheria husika, hatufichui, kuuza, kupatiana, kusambaza, wala kutuma maelezo yako ya kibinafsi kwa mhusika yeyote mwingine.

**B3. Hatua za Udhibiti wa Kiusalama**

Tunachukua hatua hitajika na mwafaka ili kuzuia uvujaji, au upotezaji, au uharibifu wa maelezo yako ya kibinafsi yanayoshughulikiwa, na pia kudumisha usalama wa maelezo ya kibinafsi, kama vile kwa kuweka sheria za kushughulikia maelezo ya kibinafsi, ufuatiliaji wa mara kwa mara, mafunzo ya mara kwa mara kwa waajiriwa katika kushughulikia maelezo ya kibinafsi, uzuiaji wizi au upotezaji wa vifaa vinavyotumika kushughulikia maelezo ya kibinafsi, na utekelezaji wa vidhibiti vya ufikiaji. Pia tunazimamia ipasavyo wanakandarasi na waajiriwa wetu wanaoshughulikia maelezo ya kibinafsi. Unaweza kupata maelezo ya ziada kuhusu hatua za kudhibiti usalama zilizowekwa kuhusiana na kushughuikia maelezo yako ya kibinafsi kwa kuwasiliana nasi kwenye Lango letu la Maombi.

**B4. Maelezo ya Marejeleo kuhusu Kuchakata Data za Kibinafsi katika Nchi za Kigeni**

Data zako za kibinafsi zinachakatwa katika EU na Marekani.

**B5. Haki za Kisheria chini ya APPI**

Ili kutumia haki zako zinazopatikana chini ya APPI tafadhali wasiliana nasi kwenye Lango letu la Maombi.

**NYONGEZA YA C: AJENTINA**

Ikiwa makazi yako ni Jamhuri ya Ajentina, tunakufahamisha kwamba SHIRIKA LA UFIKIAJI WA MAELEZO YA HADHARANI, kwa uwezo wake kama Shirika la Udhibiti la Sheria Na. 25,326, lina mamlaka ya kusikia malalamishi na madai yaliyoandikishwa na wale ambao haki zao zimeathiriwa na kukosa kuambatana na sheria zilizowekwa kuhusiana na ulinzi wa data za kibinafsi.

Shirika hili linaweka kufikiwa kama ifuatavyo:

Anwani: Av. Pte. Gral. Julio A. Roca 710, 5th floor - Autonomous City of Buenos Aires

Postal Code: C1067ABP

Nambari ya simu: (54-11) 3988-3968

Barua pepe: datospersonales@aaip.gob.ar

**NYONGEZA YA D: SINGAPOO**

Ikiwa wewe ni mkaazi wa Singapoo yafuatayo yanatumika kwako:

**D1. Ukusanyaji, matumizi na ufichuaji wa data zako za kibinafsi**

Ikiwa wewe ni mkaazi wa Singapoo na kwa idhini yako, tutakusanya, kutumia na vinginevyo kufichua data zako za kibinafsi kwa ajili ya kila moja ya malengo yaliyobainishwa kwenye kauli yetu ya faragha. Unaweza kutumia haki yako ya kuondoa idhini yako wakati wowote, lakini tafadhali kumbuka kwamba huenda tunashindwa kuendelea kukupa huduma zetu kulingana na hali na wigo wa ombi lako. Tafadhali pia kumbuka kwamba kuondoa idhini hakuathiri haki yetu ya kuendelea kukusanya, kutumia na kufichua data za kibinafsi pale ambapo ukusanyaji, matumizi na ufichuaji huo bila idhini unaruhusiwa au unahitajika chini ya sheria husika.[1]

**D2. Kutumia haki zako kama mmiliki data**

Unaweza kudhibiti data za kibinafsi ambazo tumekusanya na kutumia haki zozote kwa kuwasiliana nasi kwenye Lango letu la Maombi. Tunalenga kujibu ombi lako punde iwezekanavyo, kwa kawaida ndani ya siku 30. Tutakufahamisha mapema ikiwa hatujaweza kujibu ombi lako ndani ya siku 30, au ikiwa hatuwezi kutimiza ombi lako na sababu kwa nini.[2]

Inaporuhusiwa na sheria, tunaweza kukutoza ada ya kiutawala ili kutimiza ombi lako.

**D3. Kutuma data zako za kibinafsi hadi nchi zingine**

Ikiwa wewe ni mkaazi wa Singapoo na tumekusanya data zako, tunaweza pia kutuma data zako nje ya Singapoo mara kwa mara. Hata hivyo, kila wakati tutahakikisha data zako za kibinafsi zinaendelea kupokea kiwango cha ulinzi ambacho kinafanana na ulinzi unaotolewa na Sheria ya Singapoo ya Ulinzi wa Data za Kibinafsi ya 2012, kama vile kupitia matumizi ya ASEAN Model Contractual Clauses.

**NYONGEZA YA E – KOREA KUSINI**

Hati hii ya Nyongeza ya Wamiliki Data Wakorea inaelezea mazoea yetu kuhusiana na maelezo ya kibinafsi tunayochakata kuhusiana na uhusiano wako nasi ambapo wewe ni mmiliki data Mkorea.

**E.1 – Kutuma Maelezo ya Kibinafsi**

Tunapatiana maelezo ya kibinafsi au kupeana kazi ya kuchakata maelezo ya kibinafsi kwa wahusika wengine kama ilivyobainishwa hapa chini:

- Kupeana Maelezo ya Kibinafsi kwa Wahusika Wengine

| Jina la Mpokeaji | Malengo ya matumizi ya mpokeaji | Vipengee vya maelezo ya kibinafsi vya kutumwa kwa mpokeaji | Vipindi vya kuhifadhiwa na mpokeaji |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Tools for Humanity GmbH | Malengo yaliyoelezewa katika ilani hii katika sehemu ya 6 hapa juu. | Vipengee vilivyoelezewa katika ilani hii katika sehemu ya 5 hapa juu | Vipindi vya uhifadhi vilivyooelezewa katika ilani hii katika sehemu ya 11 hapa juu. |

- Kupeana Kazi ya Kuchakata Maelezo ya Kibinafsi kwa Wahusika Wengine:

Tafadhali pata orodha ya kazi zote za kuchakata data zilizopeanwa na kampuni husika chini ya kiungo hiki: https://www.toolsforhumanity.com/processors

Tunaweza kupeana kazi ya kuchakata maelezo yako ya kibinafsi na/au kutuma maelezo yako ya kibinafsi kwa malengo ya kuhifadhiwa na wahusika wengine nje ya Korea:

Ikiwa hautaki kutuma maelezo yako ya kibinafsi nje ya nchi, unaweza kukataa kwa kutokubaliana na utumaji wa maelezo ya kibinafsi, au kwa kutuomba kusitisha utumaji nje ya nchi, lakini ukikataa, hautaweza kutumia huduma zetu. Msingi wa kisheria wa utumaji wa maelezo ya kibinafsi nje ya nchi ulio hapa juu ni kwamba inajumuisha “kazi iliyopeanwa ya uchakataji au uhifadhi wa maelezo ya kibinafsi ambao ni wa muhimu katika kutatamisha na kutimiza mkataba wa mmiliki data” na masuala ya kisheria yamefichuliwa kwenye sera ya faragha (Kifungu cha 28-8(1)(iii) cha Sheria ya Ulinzi wa Maelezo ya Kibinafsi).

**E.2 – Kuharibu Maelezo ya Kibinafsi**

Wakati maelezo ya kibinafsi yanakuwa hayahitajiki kwa ajili ya kipindi cha uhifadhi kuisha au baada ya kufanikisha lengo la uchakataji, n.k. maelezo hayo ya kibinafsi yataharibiwa bila kuchelewa. Mchakato na mbinu ya kuharibu imebainishwa hapa chini:

1) Mchakato wa Kuharibu: Tunachagua vipengee fulani vya maelezo ya kibinafsi ambavyo vinaharibiwa, na kuviharibu kwa idhini ya DPO.

2) Mbinu ya Kuharibu: Tunaharibu maelezo ya kibinafsi yaliyorekodiwa na kuhifadhiwa kwa mfumo wa faili za kielektroniki kwa kutumia mbinu ya kiufundi (k.m. mfumo wa ngazi ya chini) ili kuhakikisha kwamba rekodi haziwezi kutolewa tena, huku maelezo ya kibinafsi yaliyorekodiwa na kuhifadhiwa kwa mfumo wa hati za makaratasi yanakatwa katwa au kuchomwa.

**E.3 – Kuhifadhi Maelezo ya Kibinafsi**

Ikiwa tunahitajika kuhifadhi maelezo yako ya kibinafsi kulingana na sheria husika, tutafanya hivyo kwa malengo yafuatayo na vipindi vifuatavyo inavyohitajika na sheria husika.

**E.4 – Haki Zako**

Unaweza kutumia haki zako zinazhusiana na maeleo ya kibinafsi dhidi yako, pamoja na ombi la kufikia, kurekebishwa au kufuta, au uahirishaji uchakataji wa, maelezo yako ya kibinafsi kama ilivyobainishwa na sheria husika ikijumuisha Sheria ya Ulinzi wa Maelezo ya Kibinafsi. Pia unaweza kutekeleza haki yako ya kuondoa idhini ya kukusanya/kutumia/kupeana maelezo ya kibinafsi, haki ya kuhamisha, na haki zinazohusiana na ufanyaji maamuzi kiotomatiki. Haki hizo pia zinaweza kutekelezwa kupitia wawakilishi wako wa kisheria au watu wengine walioidhinishwa kikamilifu.

Unaweza kutekeleza haki zozote husika zilizoelezewa hapa juu kwa kuwasiliana nasi kwenye world.org/requestportal.

**E.5 – Hatua za Kiusalama**

Tutatekeleza hatua za kiusalama za kiufundi, kimpangilio, na halisia zilizobainishwa na sheria husika za Korea ili kulinda maelezo ya kibinafsi, kama vile zile zilizoorodheshwa hapa chini:

1) Hatua za kiusimamizi: Uteuzi wa Afisa wa Ulinzi wa Data, uwekaji na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa ndani, mafunzo ya waajiriwa mara kwa mara kuhusu ulinzi wa data, n.k.;

2) Hatua za kiufundi: Usimamiaji mamlaka ya kufikia mfumo wa kuchakata maelezo ya kibinafsi, uwekaji mfumo wa kudhibiti ufikiaji, uwekaji mipango ya ulinzi, n.k.; na

3) Hatua halisia: Kuzuia ufikiaji vituo vya kuhifadhi maelezo ya kibinafsi na vifaa kama vile vyumba vya kompyuta na vyumba vya

kuhifadhi data, n.k.

**E.6 – Wasiliana Nasi**

Ikiwa una maswali na maombi yanayohusiana na faragha na ulinzi wa data, tafadhali wasiliana na Timu yetu ya Ulinzi wa Data kwa anwani dpo@world.org.

**NYONGEZA YA F – MAREKANI**

Sheria ya Faragha ya Mtumiaji ya California, kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Haki za Faragha ya California, kwa sasa haitumiki kwetu.

**NYONGEZA YA G - BRAZILI**

**G.1 Sheria Husika, Mdhibiti na Opereta**

Ikiwa unaishi nchini Brazili, ikiwa data zako za kibinafsi zilizkusanywa nchini Brazili, au ikiwa unatumia Huduma zetu nchini Brazili, sheria husika ni Sheria Na. 13,709/2018 (Sheria Jumla za Ulinzi wa Data, au “LGPD”).

**G.2 Haki ya kukataa**

Una haki ya kukataa matumizi ya data zako za kibinafsi kwa malengo ambayo hayategemei idhini ikiwa malengo hayo hayaambatani na LGPD. Ukiamua kukataa, hatutatumia tena maelezo yako ya kibinafsi ili kutengeneza na kuboresha vipengele na huduma ya Huduma zetu.

Kumbuka kwamba ukikosa tupatiana au ukikosa kuruhusu ukusanyaji au uchakataji wa data fulani za kibinafsi, inaweza kuathiri ubora wa huduma yako, huenda tukashindwa kutimiza malengo ya Huduma zetu, au huenda tukashindwa kukupa Huduma fulani.

Katika hali zingine, data zako zinaondolewa utambulisho, kumaanisha haziwezi kukutambulisha tena. Hauwezi kukataa matumizi ya data bila utambulishi kwa sababu haziruhusu utambulishwe, kama ilivyobainishwa kwenye LGPD. Tunatumia data hizi bila utambulisho ili kuboresha bidhaa na huduma zetu.

**G.3 Haki za kisheria chini ya LGPD**

Kulingana na LGPD, una haki ya kuthibitisha uwepo wa uchakataji, ufikiaji, urekebishaji, au ombi la uhamishaji wa data zilizochakatwa. Aidha, unaweza kuomba maelezo ya mashirika ya umma na kibinafsi ambayo kwa pamoja tunatumia data zako za kibinafsi. Pia unaweza kuomba maelezo kuhusiana na uwezekano wa kutopatiana idhini na madhara yake, na uombe kufutwa kwa data zilizochakatwa kwa idhini. Unaweza kuchagua maelezo yako kufutwa kwenye Programu ya World kwenye menyu ya Mipangilio.

Katika hali fulani, una haki ya kukataa au kuweka kipimo cha jinsi tunavyochakata data zako za kibinafsi, au kuondoa idhini yako, ambayo tunategemea ili kuchakata maelezo unayopatiana.

Unaweza kutekeleza haki zako chini ya LGPD kwa kuwasilisha ombi kwa DPO wetu ukitumia maelezo ya mawasiliano yaliyo katika sehemu ya H.4 hapa chini au kupitia lango letu la maombi la mtandaoni. Ukihisi kwamba haki zako hazijazingatiwa vya kutosha, unaweza kuandikisha lalamishi kwa Autoridade Nacional de Proteção de Dados Pessoais (ANPD) kwa kujaza fomu inayopatikana kwenye kiungo hiki: https://www.gov.br/anpd/pt-br/canais_atendimento/cidadao-titular-de-dados.

**G.4 Kutuma Data Zako za Kibinafsi Kimataifa**

Ikiwa LGPD inatumika kwako, na tumekusanya data zako za kibinafsi, tunaweza pia kuzituma nje ya nchi. Hata hivyo, kila wakati tutahakikisha kwamba data zako za kibinafsi zinatumwa tu hadi nchi za kigeni aukwa mashirika ya kimataifa ambayo yana kiwango cha ulinzi ambacho ni sawa na cha LGPD, kama inavyotambuliwa katika maamuzi ya kutosha uanayotolewa na ANPD. Endapo hakutakuwa na uamuzi kuhusu kutosha, tutaendelea kufuata kiwango cha ulinzi ambacho angalau ni sawa na kinachotolewa na LGPD kwa kutumia Vifungu vya Kimkataba vilivyowekwa katika kanuni za ANPD au tunapopokea idhini yako maalum ya kutuma kimataifa.

**AMBATISHO LA I – Misingi/malengo ya kisheria ya shughuli za Tools for Humanity za kuchakata data**

Watumiaji

| Kwa Nini Tunachakata Data | Ni Data Gani za Kibinafsi Zinachakatwa | Msingi wa Kisheria wa Uchakataji | Kipindi cha Kuhifadhi Data |
|---|---|---|---|
| Kutengeneza akaunti yako katika Programu ya World | Anwani ya pochi, metadata, jina la mtumiaji | Utekelezaji mkataba | Kipindi cha matumizi ya huduma au mpaka uombe data hizo zifutwe. |
| Kuhakikisha una umri unaofaa | Tarehe ya kuzaliwa | Jukumu la kisheria | Tarehe yako haswa ya kuzaliwa haihifadhiwi. Tunahifadhi tu kama umefikisha miaka 18. Tunahifadhi maelezo kwa kipindi cha matumizi ya huduma au mpaka uombe data hizo zifutwe. |
| Ili kuwezesha waasiliani wako kuwasiliana na kufanya miamala nawe kwa urahisi | Nambari ya simu | Idhini | Kipindi cha matumizi ya huduma au mpaka uombe data hizo zifutwe. |
| Ili kukuwezesha kuwasiliana na kufanya miamala na waasiliani wako kwa urahisi | Waasiliani katika kitabu cha waasiliani | Idhini | Kipindi cha matumizi ya huduma au mpaka uombe data hizo zifutwe. |
| Ili kukuonyesha vifaa vya Orb vilivyo karibu nawe | Maelezo ya Eneo | Idhini | Hadi miezi 24. |
| Ili kuzuia ulaghai katika muktadha wa kuzuia akaunti | Metadata, anwani ya IP address, kitambulisho cha Kifaa | Nia halali, haswa nia ua kuzuia aina fulani ya ulaghai (ORODHA YA AINA) | Hadi miezi 24. |
| Ili kuhakikisha huduma zinaruhusiwa katika nchi yako | Anwani ya IP, maelezo ya eneo | Jukumu la kisheria | Hadi miezi 24. |
| Ili kuonyesha pochi la umiliki wa kibinafsi na kuonyesha kiolesura cha miamala ya pochi | Anwani ya pochi, data za miamala | Utekelezaji mkataba | Hakuna maelezo ya kibinafsi yanayohifadhiwa katika muktadha huu. |
| Ili kuonyesha World ID yako ya umiliki wa kibinafsi na kuonyesha kiolesura cha uthibitishaji | Maelezo ya World ID | Utekelezaji mkataba | Hakuna maelezo ya kibinafsi yanayohifadhiwa katika muktadha huu. |
| Ili kuonyesha Stakabadhi zako za umiliki wa kibinafsi na kuonyesha kiolesura cha | Maelezo ya Stakabadhi, maelezo ya uhalali wa stakabadhi | Utekelezaji mkataba | Hakuna maelezo ya kibinafsi yanayohifadhiwa katika muktadha huu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| kushiriki Stakabadhi hizo | | | |
| Ili kuchambua na kutoa huduma zetu na kuendesha mazoesi ya tafiti za data | Data za matumizi na metadata, data za miamala za hadharani | Idhini | Hadi miezi 24. |
| Ili kuambatana na sheria husika kama vile sheria na vikwazo dhidi ya utakatishaji pesa | Data za miamala, anwani ya pochi | Jukumu la kisheria | Kipindi cha matumizi ya huduma. |
| Ili kuambatana na sheria husika kama vile kanuni za maudhui | Maudhui ya Miniapp | Jukumu la kisheria | Kipindi cha matumizi ya huduma. |
| Ili kuwezesha mawasiliano na uuzaji | Anwani ya barua pepe, arifa za papo hapo | Nia Halali | Hadi miezi 24. |
| | Mawasiliano kutoka kwako | Nia Halali | Hadi miezi 24. |
| | Maoni kutoka kwako | Nia Halali | Hadi miezi 24. |
| Kushughulikia maombi ya huduma, malalamishi na maswali yako kama mteja. | Maelezo ya mawasiliano na barua pepe au jina la wasifu wa mtandao wa kijamii ikiwa unataka kuwasiliana nasi kupitia mbinu kama hizo | Utekelezaji mkataba | |
| Ili kuhakikisha programu yako inafanya kazi vizuri | Metadata | Utekelezaji mkataba | Hadi miezi 24. |
| Ili kuthibitisha kifaa chako | Data za World ID ya Kifaa (alama ya kidole ya kifaa) | Utekelezaji mkataba | Kipindi cha matumizi ya huduma. |
| Kusuluhisha migogoro, kutatua masuala, na kutekeleza makubaliano yetu nawe, pamoja na Ilani hii ya Faragha na Sheria za Mtumiaji. | | | Kipindi cha matumizi ya huduma. |

Washirika wa kibiashara

| **Kwa Nini Tunachakata Data** | **Ni Data Gani za Kibinafsi Zinachakatwa** | **Msingi wa Kisheria wa Uchakataji** | **Kipindi cha Kuhifadhi Data** |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mawasiliano | Nambari ya simu, anwani ya barua pepe, Jina | Nia halali, yaani, nia ya kuwasiliana na washirika wa kibiashara. | Kipindi cha uhusiano wa kibiashara au mpaka uombe data hizo zifutwe. |
| Kudumisha na kudhibiti uhusiano wa kibiashara | Nambari ya simu, anwani ya barua pepe, Jina, data za kampuni | Nia halali yaani nia ya kudumisha na kudhibiti uhusiano wa kibiashara na washirika wa kibiashara. | Kipindi cha uhusiano wa kibiashara au mpaka uombe data hizo zifutwe. |
| Kutimiza majukumu ya KYC | Data za pasipoti, Data za kampuni | Jukumu la kisheria | Kipindi cha uhusiano wa kibiashara na hadi miaka 3 baada ya kusitishwa. |
| Ili kuchakata programu yako | Data za programu | Idhini na hatua kwa ombi la mmiliki data kabla ya kuingia kwenye mkataba. | Hadi miezi 3 kama chaguomsingi au muda mrefu zaidi ikiwa unakubali kuwa katika kundi la talanta. |

TFHPS20241017